**Muhtasari wa Shabaha za Laudato Si' na Hatua**

Laudato Si' husaidia taasisi yako, jumuia, au familia yako kutambua na kutekeleza majibu yako kwa Laudato Si'.

Migogoro ya kiikolojia ni " wito mkubwa wa ubadilishwaji wa ndani zaidi," ni namna ya kuyapiga darubini mahusiano yetu na Muumba wetu, na ndugu zetu. (LS 217). Ubadilishwaji au ugeuzwaji huu ni njia mojawapo ambayo hufumbuka ndani ya miezi mingi na hata miaka, huku Roho Mtakatifu akizidi kutuita kwenye ubora wa kina wa nyoyo zetu.

Katika majibu yetu kwenye ugeuzwaji huo, tunatambua kuwa " kuishi wito wetu wa kuwa walinzi wa Kazi ya mikono yake Mungu ni muhimu kwa maisha ya maadili." (LS 216). Matendo yanahitajika.

Shabaha za Laudato Si' huyaongoza matendo yetu. Huwa zinafafanua na kuujenga upya uhusiano baina yetu na makao yetu sote. Mikabala yake jumlishi huitambua mipaka yote ya kilimwengu ya mifumo ya kijamii ya uchumi na kiini cha kibinadamu cha migogoro ya kiikolojia. Shabaha hizi hutoa mwito wa mabadiliko ya kiroho na kimila ili kuufahamu ufungamano wa kiikolojia.

**Majibu kwa kilio cha Dunia** ni mwito wa kuyalinda makao yetu kwa ajili ya manufaa yetu sote, huku tukiishughulikia migogoro ya hali ya anga, upotevu wa bioanuwai, na uhimilivu wa kiikolojia kwa usawa.

*Baadhi ya hatua zilizopendekezwa kwa lengo la kutimizia shabaha hii ni pamoja na zifuatazo ( zitahitimishwa katika miezi ijayo)*

- Kuilinda hali ya anga kwa kuweka nishati ya jua, kuyakinga au kuyasetiri majengo, kununua nishati mbadala ikiwezekana, na kuweka vifaa safi ama majiko madhubuti ya kupikia au vifaa vya nyumbani kwa jumla.

- Kuilinda bionuwai kwa kuipanda miti asilia, kupanda mashamba asilia, kung'oa spishi vamizi na haribifu, kutumikiza mfumo wa kilimo unaochangia mageuzi murua na faafu ya hali ya anga na kurutubisha udongo, na kuvilinda vichavushaji.

- Kuzilinda chemchemi na njia za maji na ardhi kwa kuhakikisha kuwa kuna matumizi razini ya mbolea, kutumikiza unyunyuziaji maji wa matone na namna nyinginezo bora zaidi za unyunyuziaji maji, kuweka kinga murua kwenye njia za maji, kuepuka ujenzi wenye kuta zisizopenyeka, Kuuibua namna nzuri za utupaji taka wa mara kwa mara na kuzindua kampeni za uhifadhii, na kufuatilia mipango ya uhifadhi.

**Majibu kwa kilio cha Wanyonge** ni mwito wa kukuza haki ya kimazingira,kwa ufahamu kuwa sote tumeitwa kuulinda uhai wa binadamu tokea utungwaji wake hata mauti yake, na aina nyingine zote za maisha duniani.

*Baadhi ya hatua zilizopendekezwa kwa lengo la kutimizia shabaha hii ni pamoja na zifuatazo ( zitahitimishwa katika miezi ijayo)*

- Kuyalinda maisha upitia hafla za kielimu

- Kuanzisha huduma za KUNAWA kwa kuhakikisha kwamba kunayo maji safi, kuelimisha wanajamii kuhusu desturi bora za usafi, na kuhakikisha wanajamii mbalimbali wanapanga miradi ya KUNAWA.

- Kukuza na kuulinda uongozi asilia kwa kuhakikisha kwamba jamii za pale zinazo haki za ardhi yao na kwa kuukweza uongozi asilia.

- Kuona kwamba kuna upataji wa ardhi na hewa safi kwa kuhakikisha kuwa wanjamii wanaweza kupata mandhari hai na kwamba mazingira ya watoto ni safi na huru dhidi ya uchafuzi wa hewa.

- Kukua katika umoja na walio katika hatari zaidi za kudhuriwa kwa kufanya ukaguzi wa changamoto za jamii, kutoa mifumo ya kushughulilkia mahitaji ya msingi, na kuwa na mipango ya kushughuilkia mifumo iliyofeli

- Kugawana rasilimali na ujuzi kwa kujifundisha kutoka kwa wazee, kugawana rasilimali za kijamii, kugawana rasilimali za kifedha, na kuwa na siku za ujima katika jamii

Uchumi wa kiikolojia unatambua kuwa uchumi ni mfumo mdogo katika jamii ya kibinadamu, ambao wenyewe huwa umekitwa katika ulimwenguhai - makao yetu sote.

*Baadhi ya hatua zilizopendekezwa kwa lengo la kutimizia shabaha hii ni pamoja na zifuatazo ( zitahitimishwa katika miezi ijayo)*

- Kujenga na kuasaidia uchumi wenye manufaa kwa wote kwa kuzindua jamii za kibiashara na kununua kutoka kwa wauzaji rejareja ambao hutumia vifaa vya kukarabatiwa.

- Kuhakikisha kuwa uwekezaji wa kifedha ni adilifu na himilivu kwa kuepukana na fueli au nishati za kale, kuwekeza katika miradi yenye uwajibikaji wa kijamii, na kuteua kampuni adilifu za huduma za benki na bima.

- Kufanya manunuzi nafuu na himilivu kwa kusaidia biashara adilifu, kwa kuzingatia " mkabala wa umilikaji wa jumla wa gharama" kwa manunuzi, kuandaa orodha himilivu ya kufanyia manunuzi, na kununua kutoka kwa wauzaji rejareja wa pale.

- Kuhakikisha kuwapo kwa hadhi ya wafanyakazi kwa kuwasaidia kupata ajira bora zenye ujira na manufaa ya kuyakimu maisha yao, kusaidia katika desturi bora za usimamizi wa mashirika, kuwasaidia wale wafanyao " huduma za utoaji huduma" na kununua kutoka kwa mashirika na shughuli adilifu za kibiashara.

- kushiriki katika uchumi wa kizawadi (usio wa nipe-nikupe) kwa kufundisha maadili ya uchumi wa aina hii.

**Kukubali mitindo himilivu ya kimaisha** kumekitwa katika dhana ya utoshelevu, na kukuza urazini katika matumizi ya raslimali na nishati.

*Baadhi ya hatua zilizopendekezwa kwa lengo la kutimizia shabaha hii ni pamoja na zifuatazo ( zitahitimishwa katika miezi ijayo)*

- Kuboresha uhimilivu katika majengo kwa kuweka vitoa mwanga madhubuti zaidi, kupunguza matumizi ya kawi ya joto na uyoyozi-hewa, na kuweka mabomba yenye kumimina kwa kwa kadri.

- Kuboresha uhimilivu katika uchukuzi kwa kuongeza matumizi ya magari ya umeme ama baiskeli na kubadilisha mifumo ya kiotomatiki.

- Kuboresha uhimilivu katika lishebora kwa kupunguza uharibifu wa vyakula kabla na baada ya kununua ama kuuza, utengenezaji mbolea kwa uchafu wa mimea kama malighafi kuu, ununuzi wa bidhaa kutoka kwa wazalishaji asilia ikiwezekana, na kubadili kutoka kwa ulaji mwingi nyama hadi kwa ule unaohusu vyakula vya mimea.

- Kuboresha uhimilivu katika ununuzi na watumiaji kwa kuondoa matumizi ya sandarusi na mikebe yenye kuundwa kwa bidhaa zinazoweza kutupwa, kukarabati madhubuti mara nyingi iwezekanavyo, na kupunguza ununuzi wa bidhaa mpya

**Elimu ya kiikolojia** huhusu kuyafikiria na kuyafafanua upya mageuzi ya kimtaala na kitaasisi kwa moyo wa ikolojia fungamano ili kuwako na ufahamu wa ikolojia hii na mabadiliko katika matendo.

*Baadhi ya hatua zilizopendekezwa kwa lengo la kutimizia shabaha hii ni pamoja na zifuatazo ( zitahitimishwa katika miezi ijayo)*

- Kuzindua nafasi za mafunzo ya Laudato Si' kwa kutekeleza mfumo wa elimu ya Laudato Si' na kwa kuhakikisha kuwa wanajamii wanafahamu mfumo wa mazingira yao, sayansi na mitazamo ya kijamii kuhusu migogoro ya kiikolojia, na maadili ya kiikolojia.

- Kuhakikisha kuwa elimu inaongozwa na jamii kwa kubuni njia za kuwabadilisha waelimishaji kiikolojia, kubuni nafasi za hafla zinazoongozwa na vijana, na kuzindua namna za kuwatambua vijana hadharani kwa uongozi wao.
- Kuzifuma pamoja dhamira za Laudato Si' na mawasiliano ya jamii kwa kuwadokezea mara kwa mara kwenye magazeti na majarida na kwenye

mitandao ya kijami, na kwa kuwatia shime wanajamii kuanzisha na kuiandama Mipango ya Laudato Si'

- Kuwapo kwa upatikanaji sawa wa elimu kwa kuhakikisha kuwa makundi yasiyowakilishwa kikamilifu yamepata elimu, kuelekeza mifumo ya elimu kwa watu mbalimbali, kutoa elimu ifaayo kimila au mbadala wake, na kuhakikisha kwamba elimu inakuza hadhi na haki za kibinadamu.

**Ikolojia ya kiroho** huiopoa ruwaza ya kidini ya uumbaji wake Mungu na kuhimiza uhusiano zaidi na ulimwengu asili kwa namna ya kuajabisha, kusifia, kufurahisha na iliyojaa shukrani.

*Baadhi ya hatua zilizopendekezwa kwa lengo la kutimizia shabaha hii ni pamoja na zifuatazo ( zitahitimishwa katika miezi ijayo)*

- Kusherehekea Msimu wa Uumbaji kwa kuushikirisha Msimu huo na wa jamii nyingine, kuombea hadharani ukombozi wa kiikolojia na kijamii wakati wa msimu kama huo, kuanzisha desturi ya kuadhimisha Msimu wa Uumbaji kila mwaka, na kuchapisha taarifa za mwaka kuhusu msaada wenu kwa Msimu huo wa Uumbaji.

- Kuhimiza jamii kutafakari kuhusu dhamira za Laudato Si’ na kiongozi wa jamii kuzungumzia kuhusu dhamira hizo, kuzitalii na kuzijumuisha katika sherehe za liturjia, na kuunda miongozo ya maombi.

- Kuombea kwenye mazingira asilia kwa kuyabariki mazingira hayo kama mahali au eneo lao la kufanyia tafakuri na taamuli na kufanya mazoea ya kuombea hapo, kuandaa huduma za maombi mahali nje na wazi, na kubuni jarida la maombi, bango, au njia nyingine yoyote ile ya kurekodi na kushiriki maombi katika mazingira asilia.

**Ushirikishwaji wa jamii na hatua shirikishi** huhimiza makuzi ya tamaduni na sera ambazo huyalinda makao haya yetu sote na wote wanaoyashiriki makao haya.

*Baadhi ya hatua zilizopendekezwa kwa lengo la kutimizia shabaha hii ni pamoja na zifuatazo ( zitahitimishwa katika miezi ijayo)*

- Kutetea vyanzo vya kiikolojia na kijamii kwa kutambua sera ya kijamii na kimazingira , kuandaa hafla za ama umma au binafsi na viongozi ili kujadili masuala ya utetezi, kudumisha ukaguzi wa mara kwa mara wa sera na kuelezeana taarifa mpya miongoni mwa wanajamii, na kuwa na fursa ya kiongozi wa jamii kutoa taarifa hadharani kuhusu masuala ya utetezi.

- Kuushirikisha kwa mapana umma kwa kuandaa hafla za kiikolojia na kijamii, aghalabu kwa kutalii mfumo wa kimazingira kama kundi, na kuandikisha kwenye magazeti ya mahali penu au kutoa maoni kwenye taarifa za habari za kwenu zinazohusiana na maudhui ya Laudato Si'.

- Kwa kukuza namna za kijamii za kukabiliana na changamoto zinazofanana kwa kushirikiana na viongozi ili kung'amua njia gani ambazo Kanisa linaweza kuusaidia mfumo wenu/ programu zenu za kijamii na kiikolojia na kwa kukuza muungano wa jamii ili kujitayarisha kukabiliana na masuala ibuka ya kijamii.

- Kukuza uthabiti kwa kuchanganua njia za kimaumbile, kijamii, na kiroho ambazo jamii yako inaweza kuathiriwa na mabadiliko ya hali ya anga na upotevu wa bioanuwai na kubuni mikakati ya kujitayarisha imara kwa mabadiliko hayo, kuhakikisha kuwa majengo yametayarishwa vyema dhidi ya hari, joto au mwako, nguvu za radi, na kupwa kwa bahari, na kuhakikisha wanajamii wanaweza kusafiri hadi maeneo mengine endapo kutakuwa na dharura isababishwayo na hali ya anga.